# MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 9-11-2016

## AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 1/11/2016 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 5:00 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kisha kusoma dua la kuliombea Baraza na kuwatambulisha wageni waalikwa.

## AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 2/11/2016 KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kusoma agenda, jumla ya agenda nane zilipitiswa ili kuwa agenda halali za kikao.

## AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 3/11/2016 MASWALI YA PAPO KWA PAPO

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kwenye utaratibu wa kuuliza maswali ya papo kwa papo, muuliza swali wa kwanza Mh. Dismas Vakule (Muhinda) aliuliza kama barabara za Nyaruboza – Muhinda zimekwaishaingia kwenye mfumo wa wakala wa barabara nchini. Pia alitaka kufahamu ni lini Zahanati ya Muhinda itapatiwa usajili, na mwisho alitaka kufahamu ni lini barabara ya Muhinda – Nyakimue itafanyiwa ukarabati.

- Mwenyekiti alijibu maswali hayo kwa kusema kuwa, barabara ya Muhinda – Nyaruboa mchakato wake unaendelea na kwasasa umefikia hatua ya manunuzi.
- Kuhusu barabara ya Muhinda – Nyakimue alisema kuwa ni vyema wananchi wakaanzisha barabara hiyo kisha Halmashauri itaendeleza kama ikipata ufadhili.
- Kuhusu Zahanati ya Muhinda, utaratibu wa kuisajili ulishaanza kwasasa majibu ya usajili huo yanasubiriwa.

Muuliza swali wa pili Mh. Dickson Bunga (Mubanga) aliuliza ni kiasi gani kimepangwa kwenda kwenda kwenye vijiji husika kutoka kwenye ushuru wa Kahawa uliopatikana.

- Swali hilo lilijibiwa na Menejimenti kuwa, ushuru ambao Mh. Diwani anaulizia haupo kisheria.

Muuliza swali namba tatu Mh. Pascal Nkeyemba (Janda) aliuliza juu ya upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi. Pia alitaka kujua ni lini walimu walioandaa mitihani ya Taifa watalipwa.

- Swali hili llijibiwa na Menejimenti kuwa, malipo ya fedha za mitihani hulipwa na Wizara lakini mpaka sasa Wizara bado haijatuma fedha hizo.

Muuliza swali namba nne Mh. Moshi Bukebuke (Muyama) aliuliza juu ya ujenzi wa kituo cha polisi Kata ya Muyama, alitaka kufahamu ni lini ujenzi huo utakamilika. Pia aliuliza kuhusu kupata mlinzi wa kituo cha afya cha Muyama.

- Swali hili pia lilijibiwa na Menejimenti, kuhusiana na ujenzi wa kituo cha Polisi, Menejimenti iliomba muda ili ifuatilie utaratibu wa ujenzi wa kituo hicho.
- Kuhusu suala la mlinzi, Menejimenti ilisema kuwa Kituo cha Afya Muyama kinamilikiwa na Kijiji, Halmashauri inasaidia wataalamu tu na vifaa. Ilishauri Kamati ya Kijiji ikae kuona ni namna gani itapata mlinzi na kumlipa.

Muuliza swali namba tano Mh. Amos Ntanda (Rusaba) aliuliza juu ya utekelezaji wa Bajeti iliyopitisha uwepo wa Kituo cha Afya Rusaba.

- Swali hili lilijibiwa na Menejimenti, ilisema imelichukua swali hili na italifanyia kazi.

Muuliza swali namba sita Mh. Bugale Kituranya (Kilelema) aliuliza ni lini barabara ya Kilelema – Herushingo itatengenezwa.

- Mwenyekit alijibu swali hili kwa kusema kuwa, juhudi za makusudi zinafanyika ili kupata wafadhili ili barabara hiyo ifanyiwe kazi.

Muuliza swali namba saba Mh. Tito Fumawicha (Munyegera) aliuliza juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji, alitaka kufahamu ni lini vyanzo hivyo vitatunzwa ili kuepuka uharibifu.

- Swali hili lilijibiwa na Menejimenti kuwa, suala hili lilianza kufanyiwa kazi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Wilaya ya Kasulu. Vilevile umepatikana msaada wa Shirika la Afya Duniani ambao wameonyesha nia ya kusaidia juhudi za utunzaji wa vyanzo vya maji.

**AGIZO: Itengenezwe sheria kisha ipelekwa kwenye Vijiji.**

Muuliza swali namba nane Mh. Hamis Lukanka (Mkatanga) aliuliza juu ya mtu aliyewatapeli wananchi kwa kujifanya Mtumishi wa Halmashauri Idara ya Ardhi, alitaka kufahamu ni lini mtu huyo atachukuliwa hatua. Pia alitaka kufahamu ni lini Halmashauri itatunga sheria za mazingira ili kuzuia uharibifu wa mazingira.

- Mwenyekiti alishauri mtu huyo akamatwe hata akionekana huko vijijii.

Muulza swali namba tisa Mh. Yusufu Degede (Kinazi) aliuliza uwezekano wa Serikali kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi wa soko la Kinazi.

- Mwenyekiti alijibu kwa kusema kuwa, suala hilo limechukuliwa na litafanyiwa kazi.

**AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 4/11/2016 KUTHIITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TEREHE 13/09/2016**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari kisha nakala mbili za muhtasari huo ziliwekwa saini ili kuwa kumbukumbu halali za Halmashauri.

**AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 5/11/2016 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 13/09/2016**

Utekelezaji wa azimio namba moja ulisomwa, wajumbe waliupokea na kuridhia.

Utekelezaji wa azimio namba mbili ulisomwa, wajumbe waliupokea na kuchangia, Mh. Pascal Nkeyemba (Janda) alihoji kuhusiana na utekelezaji huo kwa kusema kuwa haujafafanuliwa vizuri.

Mwenyekiti alitolea ufafanuzi kuhusiana na suala la Waraka unaohusiana na uchaguzi wa wajumbe wa kamati za kudumu za Halmashauri, alisema kuwa Waraka huo umetolewa nchi nzima na uchaguzi utafanyika mwakani mwezi wa sita.

Utekelezaji wa azimio namba tatu ulisomwa, wajumbe waliupokea na kuchangia, Mh. Venance Kigwinya (Buhigwe) alitaka kufahamu kuhusiana na hatma ya wananchi ambao wanamiliki mashamba/viwanja kwenye eneo la Bwega na Ruheka.

Mwenyekiti alijibu kwa kusema kuwa suala hilo litashughulikiwa baadaye.

Utekelezaji wa Azimio namba nne ulisomwa, Mh. Tito Fumawicha (Munyegera) alitaka kufahamu ni kwa nini gharama ya madeni wanayodaiwa watu hao haijaainishwa.

Mwenyekiti alijibu kwa kusema kuwa, vitabu vya HW5 havikuwa na kiwango cha thamani hivyo ni vigumu kupata jumla ya fedha zinazodaiwa.

Mjumbe Mh. Pascal Nkeyemba (Janda) alihoji juu ya hatua zilizochukuliwa na Menejimenti juu ya wadaiwa wa vitabu vya ukusanyaji wa mapato, alisema kuwa hatua hizo ziko taratibu sana.

Pia alitaka kujua ni kwanini suala hili lirudishwe kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

- Menejimenti ilijibu kwa kusema kuwa, kulipeleka suala hili kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ni kufuata utaratibu kisha litaletwa tena kwenye Baraza kwa ajili ya kulipitisha.

Mjumbe Mh. Wilson Luzibila (Munzeze) alisema kuwa yaliyoandikwa sio maagizo ya kikao kwahiyo maagizo ya kikao hayakutekelezwa.

Mjumbe Mh. Venance Kigwinya (Buhigwe) alisema kuwa tatizo kubwa ni muingiliano wa maslahi kati ya Menejimenti na Waheshimiwa Madiwani, alishauri kuwa ni vyema wadaiwa wakaitwa ili wahojiwe watoe maelezo ya kwanini hali iko kama ilivyo ili ijulikane kinachoendelea.

Mwenyekiti alisema kuwa, hakuna mgongano wowote wa kimaslahi bali ni kutofautiana kwa mitazamo tu.

Mjumbe Mh. Moshi Bukebuke (Muyama) alisema kuwa anapata wasiwasi kwa kuwa Baraza halijui hata kitu lililokiamua. Alisema kuwa ana mashaka na taarifa za madeni zilizoletwa. Alihoji ni kweli Idara ya Fedha haijui thamani ya hivi vitabu.

- Menejimenti ilijibu kwa kusema kuwa, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa alishatoa mwongozo wa namna ya kufuta hasara ya Halmashauri – kwa kuwaita wadaiwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ili yakafanyike makadirio kisha yapewe baraka na Baraza.

Kikao kilikubaliana kuwa, suala hili lirudi kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ili utaratibu wa kikanuni ufuatwe.

**AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 6/11/2016 TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI**

I. KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Kamati hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea na kuijadili. Mjumbe Mh. Amos Ntanda (Rusaba) alihoji kwanini kikao cha Kamati kikae mara moja kwa rob ya mwaka.

- Menejimenti ilijibu kwa kusema kuwa, kikao kilikaa mara moja kwasababu mbalimbali zilizojitokeza.

Mjumbe Mh. Tito Fumawicha (Munyegera) alitaka kufahamu sababu zilizotumiwa kumkataa aliyependekezwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri.

Mwenyekiti alijibu kwa kusema kuwa, huo ndio uamuzi kulingana na kanuni.

II. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Kamati hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo, wajumbe waliipokea na kuipitisha.

III. KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Kamati hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuijadili, Mh. Pascal Nkeyemba (Janda) alizungumzia suala la michezo kwenye Wilaya hususani kutotolewa kwa taarifa za

utekelezaji wa kitengo cha michezo. Alitaka kujua ni kwa nini kitengo cha michezo hakitoi taarifa kwenye Baraza hili.

- Menejimenti ilijibu kwa kusema kuwa imelichukua suala hilo na kulifanyia kazi ili kulitolea taarifa baadaye.

Mjumbe Mh. Dismas Vakule (Muhinda) alitaka kufahamu juu ya suluhu ya mtumishi aliyetumia fedha za CHF. Pia alitaka kujua juu ya upimaji wa shule ya Nyaruboza.

Mjumbe Mh. Venance Kigwinya (Buhigwe) naye alitaka kufahamu kuhusu mchakato wa kupandisha hadhi shule mbili za sekondari ili kuwa shule za sekondari za juu, shule ya Buyenzi na Muyama.

- Menejimenti ilijibu kuhusu suala la Nyaruboza kwa kusema kuwa itaangalia katika bajeti inayokuja ili kupanua shule hiyo.
- Kuhusiana na shule za sekondari za juu, Menejmenti ilisema kuwa, inategemea uwezo uliopo wa kuziendesha shule hizo.

**Kikao kiliridhia shule hizo kupandishwa hadhi na kuwa shule za sekondari za juu.**

## IV. TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kamati hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuanza kujadili. Mjumbe Mh. Pascal Nkeyemba (Janda) alitaka kujua hali ya UKIMWI katika Wilaya ikoje.

Mjumbe Mh. Tito Fumawicha (Munyegera) alitaka kujua kama waathirika walioko ndani ya Halmashauri wanapata haki zao. Pia alihoji kuhusiana na matumizi ya fedha ambazo hazionekani kwenye taarifa.

- Hoja hizo zilijibiwa na Menejimenti kwa kusema kuwa, takwimu zipo japokuwa hazikuonyeshwa kwenye taarifa laikini asilimia ya maambukizi ni asilimia 3 na Buhigwe ina vituo vitatu vya kushughulikia masuala ya UKIMWI na mpaka sasa huduma zinaendelea.

Mjumbe Mh. Robisoni Ngeze (Kajana) alishauri kuwa, Idara inayohusika na UKIMWI iwe inaleta taarifa zinazojitosheleza kwenye vikao.

## AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 7/11/2016 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hakukuwa na mengineyo yaliyowasilishwa kwa Mwenyekiti.

**AGENDA: NA. BHDC/BRZ/MUHT. 8/11/2016 KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alimuomba Mkuu wa Wilaya kuzungumza na wajumbe wa kikao.

Mkuu wa Wilaya aliwashukuru wajumbe hususani Waheshimiwa Madiwani kwa kushiriki vyema kwenye uzinduzi wa wa mradi wa ujenzi wa madarasa, kisha akawataka kutobweteka katika kukamilishaujenzi huo. Alitoa taarifa kuwa Wilaya imeanza imeanza mchakato wa kujenga Hospitali ya Wilaya na inatarajia kupata ramani wiki ijayo. Aliwaomba kuunga mkono suala hilo litakapokuwa tayari.

Alitoa taarifa ya kuhusiana na mgogoro wa chama cha Ushirika Manyovu uliokuwa ukiendelea, na alihitimisha kwa kusema kuwa, hajaridhishwa na kasi iliyopo ya kuibua vyanzo vipya vya mapato. Aliitaka Menejimenti iongeze kasi kwenye suala hilo.

Baada ya Mkuu wa Wilaya kuzungumza na wajumbe, Mwenyekiti alimuahidi kutoa ushirikiano na kisha kufunga kikao mnamo saa 8:05 mchana.

**MUHTASARI HUU WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 09/11/2016 UMESAINIWA NA:**

| | |
|---|---|
| **SAINI. ……..** | **SAINI. …….** |
| **JINA KAMILI. ……** | **JINA KAMILI. ……** |
| **TAREHE. …….** | **TAREHE. …….** |
| **KATIBU.** | **MWENYEKITI.** |